


# JINSI YA KUWA MILIONEA Adhkaar Zenye Thawabu Tele

Hii ni biashara na Allah subhaanahu wataala yenye faida kubwa yenye uhakika. Mtaji wake ni muda wako na ikhlasi yako. Utavuna kila siku mamilion ya thawabu. Usikubali kuwa maskini duniani na kesho akhera. Biashara hii na Allah subhaanahu wataala ina faida kubwa na ni bora isiokua na hasara.

Haichukui muda mrefu kufanya nyiradi hizi lakini inakupa mabilioni ya thawabu na kufutwa madhambi yako

Zifuatazo ni Adhkaar ambazo Muislamu anapozisoma, atajichumia milioni za thawabu kwa muda usiozidi dakika moja kila moja (والله يضاعف لمن يشاء) Thawabu moja unalipwa mara kumi kama ilivyokuja kwenye sunnah (من قرأ حرفا من كتاب الله فله به حسنة ، و الحسنة بعشر أمثالها ، لا أقول { الم }حرف و لكن : الف حرف ، و لام حرف ، و ميم حرف

Zote zimetokana na mafunzo Sahihi katika Sunnah. Tunataraji kwenu wasomaji kuisambaza hizi dhikri kwenye group zenu za whatsapp au kuchapisha na kusambaza katika madrassa,misikiti,sehemu za kazi na kwengine utakapoweza. Fanya hivyo na utapata thawabu ya kusaidia elimu hii .Chapisha kisha uweke mahali kama dukani kwa jamaa au rafiki yako ili asambaze bure kwa wateja wake. Tuweze kushindana mambo ya kheri. Unaweza pia kuwarushia watu wako wote walio katika whatsapp yako. Hata pia mgeni yeyote akija kwako mpe copy moja.

Amesema mtume rehma na amani iwe juu yake: (صلى الله عليه وسلم) ٠ (الدال على الخير كفاعله) Mwenye kuonesha au kuelekeza kheri anapata malipo kama aliefanya.

## 1- سبحان الله وبحمده عدد خلقه ورضا نفسه وزنة عرشه ومداد كلماته) ثلاث مرات.

SubhaanaLLahi wa Bihamdihi ‘adada Khalqihi wa Ridhwaa Nafsihi wa Ziynata ‘Arshihi wa Midaada Kalimaatihi (mara 3)

Akisema hivyo atapata ujira(thawabu) mfano wa idadi ya vitu hivi.

(1)Idadi ya viumbe vyake ni vingi na vyengine hatuvijui. Hatujui viumbe vyote kikamilifu vya Allah subhaanahu wataala. Mfano ukiangalia idadi ya malaika ni wengi sana, Idadi ya mchanga jangwani ni nyingi sana, idadi tu ya samaki na species zake ni nyigi sana,

Kwa hakika Calculator yetu haiwezi kuhesabu viumbe vyote vya mwenyezi Mungu.

(2) (Ridhaa nafsihi (رضا نفسه) Allaah subhaanahu wataala pekee ndie anaejua anavioviridhia.

(3) (Zinatu arshihi (زنة عرشه)kwa maana ya uzito wa arshi yake. Uzito wa arshi ya Allah subhaanahu wataala yeye peke yake ndie anayejua na tukifanya dhikri hii tunapata thawabu idadi ya mfano wa uzito wa arshi.

(4) Midaada kalimaatihi (مداد كلماته) Kwa maana ya wino ya maneno yake. Lau tukitaka kuandika Maneno ya Allah subhaanahu wataala na tukachukua maji yote ya bahari zote ulimwenguni ikawa ndio wino, bahari zitakauka au kuisha kabla hatujamaliza kuandika maneno yote ya Allah subhaanahu wataala

## 2- الصلاة على النبي – صلى الله عليه وسلم :

**إذا صلى على النبي واحدة صلى الله عليه عشرا وحط عنه عشر خطيئات ورفع له عشر درجات**

Ukimswalia MTUME Wete Muhammad (صلى الله عليه وسلم) idadi yoyote na kila mara unafutiwa madhambi kumi na kupandishwa daraja kumi na Allah subhaanahu wataala anakupa rehma mara kumi na salamu zako zinapelekwa kwa mtume Muhammad(صلى الله عليه وسلم kwa hivyo utapiga hesabu mara ya idadi nyingi ya sala utakazo swali na utaona thawabu zake ni idadi kubwa sana.

(3)-Thawabu nyingi kwa idadi ya waumini kote ulimwenguni unapowatakia istighfar kwa maana ya msamaha na maneno yenyewe ni: (اللهم اغفر للمؤمنين والمؤمنات)

Kwa mara ya mwisho kuangalia niliona kuwa idadi ni kama ( 1500.000.000). Kwa hivyo ukiomba tu dua hii mara moja unapata thawabu hizo zote.

4- Kusema mara mia moja سبحان الله و الحمد لله و لاإله إلا الله و الله أكبر. Haya ni maneno manne lakin malipo yake ni makubwa sana. Thawabu yake ni kuwa kwa kila neno unapata mti mmoja peponi. Na haya maneno yanapendeza kwaAllah subhaanahu wataala.Na haya maneno pia ni wasia wa mtume wetu muhammad (صلى الله عليه وسلم) kwa yule anaemuuliza amfundishe maneno ya kusema.Na maneno haya pia huporomosha au kudondosha madhambi ya mja.

5- Kusema mara mia (سبحان الله) Unaandikiwa thawabu elfu moja na kufutiwa madhambi elfu moja.

6-Kusoma mara tano suratul  Fatiha الفاتحة unapata thawabu 7000 na Allah subhaanahu wataala humzidishia amtakae.

7- Amesema mtume wetu Muhammad (صلى الله عليه وسلم)  : ( قل هو الله أحد تعدل ثلث القرآن ) Kusoma suratul Ikhlasi ni sawa kwa thawabu kusoma qurani thuluthi yake. Atakaeisoma mara tatu ni kama aliekhitimisha Qurani yote.Na ukiisoma mara 12 utapata thawabu kama aliekhitisha Qurani mara nne

Tukianza kuhesabu kwa pamoja
Kwa siku khitma mara nne
Kwa mwezi4*30=120 khitma
Kwa mwaka 120*12=1440 khitma
Kwa miaka 20 1440*20=28.800 khitma

"من قرأ { قل هو الله أحد } ١٠مرات بنى الله له بيتا في الجنة .

8-Kusoma suratul Baqara البقرة kila siku. Idadi ya aya zake ni 286 na herufi zake ni 25500 or 25613 Utapata thawabu ya hizi herufi.Fadhila zake ni nyingi.

9-Maneno ukiyasema mara mia kwa siku utapata thawabu zifuatazo na hakuna atakaekuja na amali bora kukuliko illa atakaezidisha zaidi yako. Thawabu  hizi ukisema mara mia asubuhi utapata thawabu mchana kutwa na ukisema jioni utapata thawabu usiku kucha. Maneno yenyewe ni:

لا إله إلا الله وحده لاشريك له,له الملك وله الحمد وهو على كل شيء قدير

Thawabu zake ni:1-Utapata thawabu ya kuwacha huru watumwa kumi,2-Utaandikiwa thawabu mia, 3- Utafutiwa

madhambi mia, na 4- Utapewa kinga dhidi ya shetani siku yako hio hadi jioni.

Njooni tuhesabu pamoja:

Kwa siku thawabu 100

Kwa mwezi thawabu 100*30=3000

Kwa mwaka thawabu 3000*12=36000

10- سبحان الله والحمد لله ..تملأ مابين السماء والأرض

Thawabu zake ni nyingi na mfano wake inajaa baina ya mbingu na ardhi.